



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



Unapojibutafadhalitaja:

KUMB.NA.AB.53/172/01A/12

20/06/2023

YAH: TANGAZO LA KAZI.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Illemela imepokea kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/359/01B/90 cha tarehe 31 Mei 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kutokana na Kibali hicho Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Illemela anawatangazia Wananchi wote wenyewe sifa za Muundo wa kazi kwa nafasi ifuatayo:-

MTENDAJI WA MTAATARAJA III – (NAFASI 2).

1.1 Mwombaji awe na Sifa zifuatazo:-

- i. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti (**NTA LEVEL 5**) katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa Kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

1.2 Kazi na Majukumu:-

- i) Atakuwa ni Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa.
- ii) Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora Katika Mtaa.

- iii) Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mtaa
- iv) Kuwa Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa.
- v) Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu katika Mtaa
- vi) Kuandaa taarifa ya Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umasikini, njaa na kuongoza uzalishaji mali.
- vii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote nyaraka za mtaa
- viii) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika ngazi ya Mtaa.

1.3 Ngazi ya Mshahara TGS B.

MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI.

- i. Muombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.
- ii. Muombaji ni lazima awe na umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- iii. Aambatanishe nakala za nyaraka zifuatazo katika barua ya maombi:
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Maeleo binafsi (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini.
 - Picha moja (Passport size) ya hivi karibuni na jina la mhusika liandikwe nyuma ya picha hiyo.
 - Vyeti vya Taaluma/ shule na vyeti vya Mafunzo ya Vyuo.
 - Mwombaji aliyesoma nje ya nchi ahakikishe anaambatisha cheti cha Ulinganifu (Equivalent Certificate) kilichoidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA)

- Kitambulisho cha Taifa (NIDA) na kwa ambaye hana kitambulisho hicho aandike namba ya NIDA kwenye maelezo binafsi (CV)

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 04 Julai, 2023 na barua zote zitumwe kwa anuani Ifuatayo:-

***Mkurugenzi Wa Manispaa,
Halamshauri ya Manispaa,
S.L.P 735,
ILEMELA-MWANZA***

S.S.M.
Sitta S. Makunza
**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA,
ILEMELA**
